BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani,
Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI (PAC) NA KAMATI ILIYOKUWA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA NA MASHIRIKA (LAAC) KUHUSU RIPOTI YA UTEKELEZAJI WA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

## Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote, napenda kuelekeza shukurani zangu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uhai na afya njema tukaweza kukutana katika Baraza hili kwa lengo la kuendelea kuwatumikia Wananchi wa Zanzibar kwa kutekeleza majukumu yetu mbali mbali kwa niaba yao ambapo leo tupo hapa kupitia na kujadili utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, naomba nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu ili kuwasilisha mambo muhimu kuhusiana na Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC ya mwaka wa fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika,** Nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, na Mipango; Mheshimiwa Dkt. Saada Mkuya Salum, Naibu Waziri Mheshimiwa Juma Makungu Juma, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Muhasibu Mkuu wa Serikali pamoja na watendaji wengine wote wa Wizara tofauti wakiwemo Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Makatibu na Naibu Makatibu Wakuu wa Mawizara, Wakuu wa Taasisi na Mashirika ya Umma pamoja na Wakurugenzi wote

tuliobahatika kukutana na kufanya kazi nao wakati Kamati ikihitaji majibu ya hoja za CAG. Aidha, tunawashukuru kwa mashirikiano yao ya dhati kwa Kamati wakati wote tulipokuwa tukipitia Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati yetu.

**Mheshimiwa Spika,** nitakuwa sijatenda wema iwapo nitashindwa kumshukuru Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na Watendaji wake hususan wale wanaoongozana na Kamati kwa usaidizi na ufafanuzi wanaoutoa kwa Kamati yetu kwa vile bila ya michango yao isingekuwa rahisi kwa Kamati kuweza kutoa hotuba yake mbele ya Baraza hili kiurahisi na kuweza kutoa taswira halisi ya kazi iliyotekelezwa na Kamati wakati wa kuchambua utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati yetu.

**Mheshimiwa Spika,** kazi kubwa ya ukaguzi waliyoifanya hadi leo Kamati ya PAC ikapata wasaa wa kukaa na Watendaji wa Taasisi tofauti za Serikali ni mafanikio makubwa katika utekelezaji na uimarishaji wa Utawala Bora katika nchi yetu. Kwa mnasaba huo, kwa kweli kukosekana kuwepo kwa kazi ya Mkaguzi, kazi ya Kamati ya PAC Waswahili husema hainogi.

**Mheshimwa Spika**, napenda pia kutoa shukurani maalum kwa Katibu wa Baraza Ndugu Raya Issa Msellem, Wakurugenzi wake, Mratibu wa Kamati pamoja na watendaji wote wa Afisi ya Baraza kwa maelekezo na ushauri wao kwa Kamati wakati wote wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee kabisa napenda kutoa shukurani za dhati kwa Wajumbe wenzangu wa Kamati ya PAC kwa kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ushirikiano wa hali ya juu.

**Mheshimiwa Spika**, Wajumbe hawa wamekuwa wakishiriki mijadala ya vikao vya Kamati kwa umakini mkubwa na kutumia vyema Elimu, Taaluma, Uzoefu na Vipaji vyao katika kufanya uchambuzi wa kina wa taarifa za Hesabu pamoja na taarifa nyengine zinazoletwa katika Kamati, na kutoa ushauri ambao umeifanya kazi ya Kamati hii kuwa

nyepesi. Nawashukuru pia Makatibu wa Kamati hii kwa kuratibu na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Kamati.

**Mheshimwa Spika**, kutokana na umuhimu wao, naomba kuwatambua Wajumbe na Makatibu wetu wa Kamati kama ifuatavyo:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Juma Ali Khatib | - | Mwenyekiti; |
| 2. | Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | - | Makamo Mwenyekiti; |
| 3. | Mhe. Shadya Suleiman Mohammed | - | Mjumbe; |
| 4. | Mhe. Miraji Khamis Mussa | - | Mjumbe; |
| 5. | Mhe. Mohammed Ahmada Salum | - | Mjumbe; |
| 6. | Mhe. Jamal Kassim Ali | - | Mjumbe; |
| 7. | Mhe. Bakar Hamad Bakar | - | Mjumbe; |
| 8. | Mhe. Kombo Mwinyi Shehe | - | Mjumbe; |
| 9. | Ndg. Said Khamis Ramadhan | - | Katibu; |
| 10. | Ndg. Maryam Haji Ali | - | Katibu; |
| 11. | Ndg. Famta Omar Ali | - | Katibu; |
| 12. | Ndg. Adam Maulid Simai | - | Katibu; |
| 13. | Ndg. Nassor Mdachi Mwinyi | - | Mkaguzi - Afisi ya Mdhibiti; |
| 14. | Ndg. Shehe Abdalla Ali | - | Mkaguzi - Afisi ya Mdhibiti;na |
| 15. | Ndg. Ramadhan Iddi Hassan | - | Mkaguzi - Afisi ya Mdhibiti; |

**Mheshimiwa Spika**, kwa heshima kubwa na kwa kuzingatia msingi wa Kanuni ya 109(17) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2020, nimesimama mbele ya Baraza lako Tukufu ili kusema machache kati ya mengi juu ya mambo muhimu yanayohusu Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC ya mwaka wa fedha 2020/2021 iliyowasilishwa hivi punde na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango mbele ya Baraza hili.

**Mheshimiwa Spika**, itakumbukwa kuwa Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 iliwasilishwa mbele ya Baraza lako Tukufu, kutokana na ripoti hiyo, Kamati ya PAC ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo mengi katika Ripoti hiyo ambayo yaliyotokana na ufuatiliaji wa Ripoti Sita za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Ripoti hizo ni:-

1. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi

wa Mifumo ya TEHAMA kwa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia Tarehe 30 Juni, 2021;

2. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Tawala za Mikoa, Mamlaka Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia Tarehe 30 Juni, 2021;
3. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia Tarehe 30 Juni, 2021;
4. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Hesabu za Mashirika na Taasisi Zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia Tarehe 30 Juni, 2021; na
5. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2021.
6. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi Maalum wa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2021.

**Mheshimiwa Spika,** katika ufuatiliaji wa majibu mbele ya Kamati na Taasisi tofauti za Serikali, Kamati ya PAC imegundua kuna hatua kubwa iliyochukuliwa na Taasisi hizo katika utekelezaji wa hoja zilizoibuliwa katika Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Kamati inathubutu kueleza hivyo kutokana na uwepo wa asilimia ya kuridhisha inayotokana na majibu na vielelezo vilivyotolewa na Watendaji kuthibitisha utendaji wao. Hali hiyo imepelekea hoja kadhaa kuondolewa na Kamati na nyengine kumuelekeza Mkaguzi kwenda kujiridhisha.

**Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa hoja ambazo Kamati iliamua kuziondoa ni hoja nambari 5.5.1.2 inayohusisana na kuchelewa kufika kwa gari iliyonunuliwa shilingi 58,373,700 kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya iliyohitaji

upatikanaji wa gari kwa ajili ya shughuli muhimu za Mamlaka. Gari hiyo, tayari imeshanunuliwa na inatumika kwa maslahi ya Mamlaka na kupunguza changamoto ya usafiri katika utendaji wa kila siku. Aidha, hoja nambari 5.2.1.5 inayohusiana na kutokuwepo kwa 'strong room' ya kuhifadhia fedha za mapato ya sokoni, Kamati imeamua kuiondoa hoja hiyo kwa vile malipo yote yanafanywa kupitia Mfumo wa malipo ya mapato ya Serikali "ZanMalipo'.

**Mheshimiwa Spika,** kadhalika, Kamati imebaini kwamba mikataba mingi ambayo inaandaliwa na Taasisi za Serikali inawasilishwa katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya kupatiwa ushauri wa kisheria pamoja na kutimiza matakwa ya Kifungu cha 27(3) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba tayari Serikali imeshaandaa mpango wa kuuimarisha Mtaji wa Benki yetu ya Watu wa Zanzibar ili uweze kuongeza ushindani kwa Benki nyengine ziliopo ndani na nje ya Zanzibar. Kwa vile Benki hiyo ni Benki ya Serikali, Mpango huo utatekelezwa kwa kuzingatia maelekezo yatakayotolewa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya utekelezaji mzuri uliofanywa na Taasisi hizo za Serikali bado Watendaji wa Taasisi hizo wanahitajika kujirekebisha zaidi katika utekelezaji wa mambo yafuatayo:

**1. Uimarishaji wa huduma kwa Mteja (Bank customer care).**

**Mhesmiwa Spika,** tangu Zanzibar ipate uhuru wake mwaka 1964, kumekuwa na ongezeko kubwa la uanzishwaji Matawi ya benki tofauti kutoka nje ya Zanzibar. Jambo linalopelekea kuwepo kwa ushindani katika huduma zinazotolewa na Benki husika. Kamati yetu imebaini kuwa bado huduma kwa Mteja zinazotolewa na Benki ya Watu wa Zanzibar hazijatuliza kiu ya Wazanzibar waliowengi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imegundua kuwa Watendaji wa Benki ya Watu wa Zanzibar bado hawajaamka ipasavyo kuchangamkia fursa za kibiashara ziliopo hususan za kuwa wepesi katika ukamilishaji wa taratibu za utoaji mikopo kwa Wateja wake. Kwa

mnasaba huo, Serikali inahitaji kuandaa Mpango madhubuti utakaohakikisha fursa za kibishara zinazojitokeza zinafikiwa haraka iwezekanavyo kabla ya Benki nyengine ziliopo nchini.

2. **Kutokurudishwa kwa gari iliyoazimwa kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya PAC ilipokuwa ikipitia hoja nambari 5.2.10.4 ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii inayohusiana na kuazimwa gari la mfuko kwa kipindi kisichojulikana, Kamati yetu imegundua kuwa gari inayomilikiwa na Mfuko huo imechukuliwa kinyume na utaratibu kwa takriban miaka miwili hivi sasa na kupelekwa kwenye Taasisi nyengine ya Serikali bila ya kurudishwa katika Mfuko.

**Mheshimiwa Spika,** wakati gari hiyo inachukuliwa na Serikali, ilikuwa ni gari mpya ambayo ilitumiwa si zaidi ya miezi minne ambayo uchukuwaji uliofanyika haukufuata utaratibu wa Sheria ziliopo, licha ya Kamati kubaini kuwepo kwa upungufu wa gari kwa matumizi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa vile changamoto ya upungufu wa gari kwa Viongozi wetu adhimu hivi sasa umeondoka, Kamati yetu inapendekeza kufanyike tathmini ya uzima wa gari hiyo ili iweze kurudishwa kwa Wamiliki wake, vyenginevyo ni busara kwa Serikali kuwatafutia ZSSF gari nyengine mpya kufidia usafiri waliokuwa nao awali ambao ulilenga kutumika ipasavyo kwa shughuli za Mfuko.

3. **Ufutwaji wa Madeni ya Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) kinyume na utaratibu**

**Mheshimiwa Spika,** wakati Kamati inafanya uchunguzi wake katika utekelezaji wa hoja nambari 5.3.2.4 inayohusiana na kutokuoneshwa kwa wadaiwa wa Miradi ya Uwekezaji katika Hesabu za Mwisho wa Mwaka Shilingi USD 387,308. Kamati ya PAC imebaini kwamba Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) ya maamuzi kinyume na utaratibu wa kufuta baadhi ya madeni ya muda mrefu ambayo hayawezi kulipika. Kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Namba 12 ya mwaka 2016 inaelekeza kwamba madeni ya muda mrefu na yasiyoweza

kulipika hutakiwa kupelekwa katika Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi ili yaweze kufanyiwa uhakiki na hatimae kuwasilishwa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango na kumalizia Baraza la Wawakilishi kwa maamuzi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa vile Kamati imebaini kwamba ufutaji wa madeni ulifanyika kinyume na utaratibu, ni busara kwa Mamlaka hii kuwasilisha Bodi madeni hayo kwa ajili ya kupitiwa na hatimae kufuata utarabu unaohitajika kwa mujibu wa sheria ili yaweze kuondolewa katika orodha ya madeni ya Mamlaka yao.

### 4. Kutopatikana kwa taarifa za maombi ya msamaha wa kodi katika Mfumo wa ZIPA

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa utekelezaji wa hoja nambari 5.3.2.1 inayohusiana na kutokuboreshwa kwa mfumo wa kuhifadhia Taarifa za Miradi, Kamati ya PAC imegundua kuwa kwa muda mrefu sasa Mfumo wa uendeshaji wa kituo cha "One Stop Centre) hausomani na utaratibu mzima wa utoaji wa msamaha ya kodi unaofanywa na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango na kupelekea changamoto katika uwasilishaji wa maombi ya msamaha wa kodi hizo.

**Mheshimiwa Spika,** hali hiyo haileti taswira nzuri katika utendaji wa Taasisi kubwa za Serikali ikiwemo Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA). Kwa mnsaba huo, Kamati ya PAC inapendekeza kwamba ZIPA ishirikiane kwa karibu na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuandaa Mpango rafiki utakaohakikisha taarifa sahihi za misamaha ya kodi inapatikana kwa haraka na kwa usahihi wake unaotakiwa.

### 5. Kukosekana kwa baadhi ya vielelezo

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa kazi za uchunguzi hushindwa kufanyika kwa ufanisi kutokana na ukosefu wa vielelezo. Hili limebainika wakati Kamati inapitia utekelezaji wa hoja nambari 5.3.2.2 inayohusiana na dosari zilizobainika katika matumizi ya maeneo Huru ya Vitega Uchumi Maruhubi na Amani.

**Mheshimiwa Spika,** wakati Kamati yetu inachunguza hoja hii, ilibaini kuwa kuna gari chakavu na za muda mrefu zilizopo eneo la Maruhubi zinahitaji kuuzwa kwa mujibu wa

utaratibu wa Sheria ya Fedha na Sheria ya Ununuzi. Hata hivyo, ushauri wa Kamati umeshindwa kutekelezwa kikamilifu na Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa vile haikuwa na kielelezo kinachoonesha 'chasis' namba ikiwa ni kielelezo muhimu kinachothibitisha uhalisia na uhalali wa gari husika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya PAC inaendelea kuishauri Serikali kwamba Mamlaka ya Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) ihakikishe inafuatilia na kuviweka vizuri vielelezo vyote vinavyohusiana na umiliki wa mali zao sio tu kwa vyombo vya moto bali pia mali nyengine za Mamlaka hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** hali kama hiyo imejitokeza pia wakati Kamati yetu inapitia utekelezaji wa hoja nambari 5.1.13.1 ya madeni yaliyohakikiwa na yanayostahiki kulipwa ya shilingi 89,194,001 kwa Baraza la Mji Kaskazini 'B' ambapo Kamati imeshindwa kuiondoa hoja ya Mkaguzi kwa vile hakuna kielelezo cha barua inayothibitisha uwepo wa ridhaa ya ufutwaji wa deni la shilingi milioni 108 kwa Kampuni ya Ujenzi ya Trident iliyozuiliwa kuendelea na kazi ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha kifusi kutoka Donge Mbiji hadi Chechele.

**Mheshimiwa Spika,** awali, Kamati ilielezwa kwamba kufuatia hatua ya makusudi iliyochukuliwa na Serikali ya kuamua kuyalipa madeni halali ya Serikali baada ya kuhakikiwa na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kampuni hiyo ilipofanya mazungumzo na Baraza la Mji Kaskazini 'B' ilieleza kwamba kampuni imeshavunjwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipodai kupatiwa kielelezo, Baraza lilieleza kwamba alisema kwa mdomo, kwa mnasaba huo, Kamati imeshindwa kuiondoa hoja hiyo hadi pale Baraza litakapoleta barua husika kwa kuhofia kwamba kampuni hiyo isije kuibuka baadae na kuleta malalamiko Serikalini kudai haki zake.

**7. Kutokutekeleza kwa baadhi ya Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika,** ikumbukwe kwamba Kamati ya PAC iliwasilisha mapendekezo yake kuhusiana na kukwama kwa utekelezaji wa mradi wa maendeleo ya uondoaji wa maji

machafu katika bwawa la Mwantenga. Hata hivyo, utekelezaji wake bado unasuasua hasa ukizingatia fedha zilizotengwa kwa awamu ya mwanzo hazikuweza kutumika ipasavyo na kupelekea kurudishwa kwa wafadhili wa mradi huo.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya kuwepo kwa changamoto hiyo, tayari Serikali imeshaandaa mpango wa kukamilisha utekelezaji wa mradi huo utakaofanywa kupitia mradi mwengine wa BIGZ ambapo hadi kamati inapokea majibu ya mapendekezo iliyowasilisha Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango shughuli za kuendeleza ujenzi wa Bwawa hilo bado hazijaanza kwa vile mradi wa BIGZ umeanza utekelezaji wake katika maeneo mengine.

**Mheshimiwa Spika,** kwa vile utekelezaji wake umekuwa wa muda mrefu, Kamati ya PAC inaendelea kusisitiza kwamba Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuchukua juhudi za makusudi kuhakikisha uendelezaji wa ujenzi wa Bwawa hilo unakamilika haraka iwezekanavyo ili kuwaondoshea Wananchi changamoto ya kutuwama maji machafu katika maeneo yaliyozunguka bwawa hilo.

**8. Kutokuwepo kwa wataalamu wa TEHAMA katika Baraza la Mji la Kaskazini 'B'**

**Mheshimiwa Spika,** kama tunavyofahamu kuwa shughuli za kiutendaji ulimwengine zinatekelezwa kwa urahisi zaidi kwa kutumia Mifumo ya TEHAMA ambayo hutekelezwa na taasisi husika iwapo kutakuwa na wataamu wenye uweledi wa masuala ya TEHAMA.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutathmini utekelezaji wa pendekezo la Kamati yetu la kuwepo kwa wataalamu wa TEHAMA katika Baraza hili, imebainika kwamba Baraza la Mji la Kaskazini 'B' haina wataalamu wake wa TEHAMA wanaotumika kutekeleza shughuli za Baraza hilo hususan za ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Lakushangaza, Baraza la Mji Kaskazini 'B' hutumia Wataalamu wa TEHAMA kutoka Wizarani. Hali hiyo, hupelekea kukosekana kwa utatuzi wa haraka pale inapojitokeza hitilafu ya kimifumo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kusisitiza kwamba upatikanaji wa wataalamu wa TEHAMA katika Baraza la Mji la Kaskazini 'B' ni suala la msingi. Hivyo, Baraza lichukue hatua zifaazo kuhakikisha inakuwa na wataalamu wake na sio kutegemea wataalamu

wa TEHAMA kutoka Wizarani.

**9. Uanzishwaji wa Mifumo ya TEHAMA bila ya kufanyika kwa upembuzi yakinifu**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imekuwa na nia njema katika uanzishwaji wa Mifumo ya TEHAMA ili kurahisisha kazi na kuweka ufanisi zaidi kwenye kutekeleza majukumu yake, takriban sehemu nyingi katika Wizara, Taasisi za Serikali pamoja na Mashirika ya Umma huanzisha Mifumo kwa gharam kubwa bila kufanyika upembuzi yakinifu ili kujua mahitaji halisi, hii hupelekea mifumo mingi kushindwa kufanya kazi na mengine huachwa bila maelezo sahihi kutoka kwa Wataalam. Kamati ya PAC inaishauri Serikali kuwa na utaratibu wa kufanya upembezi yakinifu katika hatua za awali ili kuepusha matumizi yasio na tija. Ni matumaini ya Kamati yetu kwamba endapo hilo litatekelezwa, Serikali itaondokana na uanzishwaji wa Mifumo kiholela na isiyoweza kufanya iliyokusudiwa.

**Hitimisho**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya PAC imebaini kuwa kuna hoja nyingi ambazo zinaingizwa katika Ripoti ya Mdhibiti kimsingi zinaweza kuepukwa katika hatua za awali hususan kwa kutumia Wakaguzi wa ndani wanapotekeleza majukumu yao ipasavyo. Kwa msingi huo, Kamati yetu inaitaka Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani (Internal Auditor General) kuzidisha kasi ya kazi kwa Wakaguzi wake wa ndani ili kuzisaidia Wizara, Mashirika na Taasisi za Umma kupunguza au kuondosha hoja sizizo za lazima.

**Mheshimiwa Spika,** Kiujumla, Kamati yetu kwa kiasi kikubwa imebaini kwamba baadhi ya Maoni, Ushauri na Mapendekezo iliyoyawasilisha kwa Wizara husika yametekelezwa kwa asilimia mia moja (100%), mengine hayajatekelezwa kikamilifu na mengine yanahitaji muda katika kukamilisha utekelezaji wake. Kwa mnasaba huo, Kamati yetu itaendelea kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo hayo ili kubaini kwamba yametekelezwa kama yalivyoelezwa na Watendaji wa Wizara kupitia majibu waliyoyawasilisha kwa Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho kabisa, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa

Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii. Kadhalika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya PAC kwa kuniteua na kuniamini kuisoma ripoti hii.

**Mheshimiwa Spika,** Sasa naomba nichukue fursa hii kwa mara nyengine nikuombeni Waheshimiwa Wajumbe muijadili, mutoe ushauri pamoja na mapendekezo yenu na hatimae muunge mkono utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo yaliyowasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kueleza hayo machache, Kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali, naunga mkono utekelezaji uliowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango.**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

Ahsante sana,

…………………

**Mheshimiwa Juma Ali Khatib,**
Mwenyekiti,
Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali,
BARAZA LA WAWAKILISHI,
ZANZIBAR.